# Adapt 2 Live: Wito wa Makabiliano na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Njia ya Ujasiri, Haki na Yanayoongozwa na Waafrika

**Sisi, mashirika na wabia tuliotia saini hapa, tumeungana katika kampeni ya Adapt 2 Live ili kuendeleza ajenda ya ustahimilivu na makabiliano na mabadiliko ya tabianchi kwa njia ya haki, yenye ufadhili wa kutosha na inayolenga watu wa Afrika.**

Makabiliano si chaguo, ni sharti la kufa au kupona. Majanga ya tabianchi yanavyozidi kuongezeka,, mamilioni ya watu katika bara hili wanakufa, kupoteza makazi, afya, maji, mifumo ya chakula, na turathi za kitamaduni. Licha ya hayo, shughuli za makabiliano hazina ufadhili wa kutosha, hazieleweki, na hazipewi kipaumbele katika mipango na utekelezaji katika ngazi za kimataifa na kitaifa.

Bara la Afrika limefikia maamuzi ya muhimu. Tayari suluhu mbalimbali zipo kote kwenye bara, zinazotokana na hatua za jamii, uvumbuzi wa ndani, maarifa asilia, mikakati inayotegemea mazingira, na maendeleo ya kisayansi. Sasa ni wakati wa kuboresha na kufadhili suluhisho hizi za muktadha mahususi kwa kuzingatia dharura, ujumuishaji, na uadilifu ili kuhakikisha ustawi na heshima kwa wote.

## Sababu za Kuchukua Hatua

Afrika huchangia chini ya 4% ya uzalishaji wa gesijoto ulimwenguni lakini inaathirika kwa njia isiyo sawa kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kuanzia ukame wa muda mrefu na kuongezeka kwa halijoto hadi mafuriko hatari na mkurupuko wa magonjwa, bara linakabiliwa na athari nyingi kuhusu usalama wa chakula, upatikanaji wa maji, na afya ya umma. Riziki zinazotegemea sana mazingira zinazojumuisha ufugaji, kilimo cha mimea na vyanzo vya asili vya maji zote zimeathiriwa. Mabadiliko ya tabianchi huzidisha ukosefu wa usawa, kuhamisha jamii, na kutishia amani na maendeleo katika bara lote.

Hatua za makabiliano zinazosababisha ustawi badala tu ya maisha duni ni muhimu, si kama nguzo ya pili ya kupunguza athari, lakini kama ajenda kuu, inayozingatia hai, kuwalinda watu, kukuza ustahimilivu, na kuhakikisha haki ya kustawi katika matukio ya mabadiliko ya tabianchi.

## Matakwa Yetu

Tunatoa wito kwa serikali za Afrika, mashirika ya kimaeneo, taasisi za kifedha ulimwenguni, na wahusika wa tabianchi kuchukua hatua za dharura katika masuala yafuatayo:

**1. Kuongeza Fedha za Hatua Bora za Makabiliano na Tabianchi Sasa**

- Kuziba pengo la fedha za hatua za makabiliano kwa kuhakikisha **ufadhili unaoweza kutabirika, kupatikana na kutegemea ruzuku** ulio wa ziada kwa kweli na unaofikia jamii zilizoathirika zaidi.
- Kuwekea kipaumbele uwekezaji katika masuala ya **usalama wa chakula, upatikanaji wa maji na mifumo ya afya ya umma inayostahimili tabianchi**.
- Kutimiza na kuongeza ahadi kwa **Hasara na Uharibifu**, na kuhakikisha kuwa nchi za Afrika haziingii katika ufadhili wa madeni.
- Kuongeza mtiririko wa Usaidizi Rasmi wa Maendeleo (ODA, Official Development Assistance) ili kusaidia mipango ya ustahimilivu ya muda mrefu barani Afrika.

**2. Kuendeleza Suluhisho Zinazotokana na Wenyeji**

- Kutambua na kufadhili **mifumo ya kiasili ya maarifa**, **desturi zinazotegemea jamii**, na **uvumbuzi wa kimaeneo** uliothibitishwa, katika muktadha mahususi na endelevu.
- Kuthamini, kurekodi na **kujumuisha mifumo ya maarifa ya wenyeji** na **desturi** pamoja na mifumo mikuu ya kisayansi, kwa kuitambua kama chanzo cha uvumbuzi na suluhisho za tabianchi.
- Kuhakikisha kuwa mipango na sera za makabiliano **zinalenga maarifa, haki na uongozi wa Wenyeji**, wanawake na jamii za mstari wa mbele.

**3. Kukuza Mwiingiliano wa Maarifa ya Jadi, Sayansi na Teknolojia**

- Kuwezesha **uasili na maendeleo ya teknolojia** ili kuboresha na kuendeleza maarifa ya eneo, huku tukihakikisha umiliki wa pamoja au umiliki wa eneo ili haki zisikiukwe katika mchakato huo
- Kuwekeza katika **miundo mahuluti** inayojumlisha mifumo dijitali ya maonyo ya mapema, data ya kisayansi, mbinu zinazotegemea mazingira, na desturi za jadi za hatua za makabiliano zinazoweza kuboreshwa na zinazomilikiwa na jamii.

**4. Kulinda Watu, Mazingira na Ardhi**

- Kulinda na kurejesha **mifumo ikolojia na bayoanuai** kama kinga muhimu kwa jamii na makazi ya binadamu dhidi ya hatari za tabianchi.
- Kutekeleza **mageuzi ya umiliki wa mashamba yanayodumisha Haki za wenyeji** ili kuzuia kupotea kwa riziki, kuhama na unyanyasaji kupitia miradi ya makabiliano na

tabianchi huku tukitambua haki za wanawake na vijana za umiliki wa mashamba.

- Kutekeleza **Michakato Isiyolipishwa, ya mapema, na yenye Idhini ya Busara (FPIC)** na kuweka ulinzi wa jamii na mazingira katika mipango yote ya maano.

**5. Kuhakikisha Usimamizi Jumuishi wa Hatua za Makabiliano**

- **Usawa wa jinsia, ujumuishaji wa walio na ulemavu na uongozi wa kawaida wa vijana** katika mchakato wote wa sera ya hatua za makabiliano.
- Kuhakikisha **ushiriki muhimu** kwa jumuiya katika viwango vyote—kuanzia mipango ya makabiliano ya eneo hadi mifumo ya kitaifa na kimataifa.
- Kuimarisha uwazi, uwajibikaji na umiliki wa Waafrika katika fursa za kufanya maamuzi kuhusu tabianchi.

**Misingi Yetu**

**Kampeni ya Adapt 2 Live imejengwa kwa nguzo tatu:**

- **Usalama wa Chakula:** Kampeni hii inaendeleza ikolojia ya kilimo, kilimo bora, na mifumo ya mbegu na chakula inayodhibitiwa na wakulima inayoimarisha afya ya udongo, bayoanuai na kujitegemea kwa jamii. Inahimiza mifumo ya chakula bora, ya bei nafuu, inayofaa eneo, na kuongozwa na wakulima wadogowadogo, hasa wanawake na vijana.
- **Usalama wa Maji:** Adapt 2 Live inahimiza usimamizi wa maji unaolenga jamii na miundombinu ya maji inayostahimili tabianchi, ikiwemo utekaji wa maji ya mvua, uasilishaji wa ardhi oevu na hifadhi inayotegemea mazingira. Kampeni hiyo pia inahimiza ufikiaji sawa wa maji salama, hasa kwa jamii za mashinani, zisizo rasmi na zilizotengwa.
- **Afya na Ustahimilivu wa Tabianchi:** Kampeni inatoa wito wa uwekezaji katika mifumo ya afya ya eneo ili kujiandaa na kushughulikia hatari za afya zinazotokana na tabianchi kama vile vipindi vya joto kali, magonjwa yanayoenezwa na wadudu na kiwewe. Hii inajumuisha huduma za afya ya akili, vituo vya afya vya kuhamishwa na kujumuisha afya katika mipango ya kitaifa ya hatua za makabiliano na tabianchi.
- **Ardhi, Watu na Makazi:** Kampeni inasisitiza umuhimu wa mageuzi endelevu ya udhibiti wa ardhi yanayokuza riziki zinazofaa jamii na zinazohifadhi ardhi, hali inayopunguza hatari kwa makazi ya watu, kadri idadi ya watu ulimwenguni inavyoongezeka.

**Vipaumbele vya Jumla**

Adapt 2 Live imejikita katika vipaumbele vya jumla ambavyo lazima vijumuishwa katika juhudi zote za makabiliano na mabadiliko ya tabianchi. Vipaumbele hivi ni pamoja na:

- **Mifumo ya maonyo ya mapema kwenye jamii na utayari wa majanga** inayowezesha jumuiya zilizo hatarini kwa kuzipa zana na maarifa ili kukisia na kushughulikia majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.
- **Ulinzi wa mfumo wa ikolojia na bayoanuai**, unaohakikisha kuwa hatua za makabiliano zinaendana na mazingira na zinaimarisha mifumo asili ya ulinzi wa sayari.
- **Ujumuishaji wa jinsia, usawa na jamii**, kutambua kuwa lazima hatua za makabiliano zipinge ukosefu wa usawa katika mfumo na kuimarisha uongozi wa wanawake, vijana, Wenyeji, watu wanaoishi na ulemavu, na makundi mengine yaliyotengwa.
- **Ardhi na Haki za Wenyeji**, ambazo ni muhimu kwa hatua za makabiliano kwa njia ya haki na kudumu. Umiliki salama wa ardhi na heshima kwa miundo ya usimamizi huhakikisha kuwa jumuiya zinaweza kusimamia rasilimali zake na kulinda musktabali.
- **Mamlaka ya makabiliano,** yanayoangazia hatua za makabiliano na njia zinazobuniwa, kutekelezwa na kuongozwa na jumuiya na nchi za Afrika, zenye mamlaka kamili kwa mifumo ya chakula, ardhi, maji na nyenzo nyingine za kiasili.

**Mustakabali wa Haki wa Hatua za Makabiliano Unawezekana**

Tunakataa mbinu za kiutawala, ukandamizaji au za dhuluma kwa hatua za makabiliano zinazosababisha madhara na athari za kikoloni, kuongeza madeni, au kunyamazisha jumuiya zilizoathirika zaidi. Tunathibitisha kuwa hatua za makabiliano katika bara la Afrika lazima ziwe **Zinaongozwa na Waafrika, zinajumuisha wanawake, zinategemea wenyeji na zinaendeshwa na jumuiya**.

Huu ni mwito wetu wa kuchukua hatua: **hatua za makabiliano zinazolinda, kuimarisha na kuwezesha. Hatua za makabiliano zinazoturuhusu kuishi maisha yasiyo duni, bali kuishi kwa heshima, utawala na haki.**

**Jiunge Nasi**

Tunazihimiza serikali, taasisi za fedha, mashirika ya utafiti, mashirika ya kiraia na viongozi wa jumuiya kuidhinisha na kutekeleza kanuni za Adapt 2 Live. Hebu tujenge mustakabali ambapo **Bara la Afrika linabuni masharti yake**, yanayoongozwa na watu wake, tamaduni zake na mamlaka yake.

**Jisajili. Simama. Adapt 2 Live.**

**Kiungo cha Kujisajili:** https://docs.google.com/forms/d/e/1FAIpQLSfyWA23ar0HR244oIU9V3ZEbID6-2J8YbG4FEK9LC2S6doJkA/viewform?usp=sharing&ouid=102997255604713067863

POWER SHIFT AFRICA

SFI SUSTAINABLE FUTURES INITIATIVE

AFREDA TANZANIA

CFE CARE FOR ENVIRONMENT For a safe world

SUHUCAM

GIFSEP Global Initiative for Food Security and Ecosystem Preservation

AFRICAN VOICES FOR AFRICA'S FORESTS

SYND STRATEGIC YOUTH NETWORK FOR DEVELOPMENT

ALEXANDRA WATER WARRIORS

GTN GRASSROOTS TRANSFORMING NETWORK Empowering Grassroot Communities, Transforming Lives

HAKI NAWIRI Afrika

RECONCILE

RESEED

WoGEM UGANDA WOMEN FOR GREEN ECONOMY MOVEMENT UGANDA

RESOURCE AFRICA

KCCWG KENYA CLIMATE CHANGE WORKING GROUP Uniting voices and action on climate change

Nalala Tree Foundation

The Nomad Child Foundation SPARKING CHANGE, IGNITING HOPE

BARINGO INDIGENOUS PEOPLES' ORGANIZATION

GREEN GLOBE ORGANISATION

Nature Gives Back